Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 03 Issue: 01 | February-2024

EAJK

# Matumizi ya Umajazi wa Kitashtiti katika Usawiri wa Wahusika na Maudhui katika Riwaya: Mfano wa Riwaya ya *Tumaini*

**Author**
**Dave Bowen**
**Email:** tbowenza@yahoo.com

**Chuo Kikuu cha Kabarak, Kenya.**

**Cite this article in APA**
Bowen, D. (2024). Matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika usawiri wa wahusika na maudhui katika riwaya: Mfano wa riwaya ya *Tumaini*. *Eastern Africa journal of kiswahili*, *3*(1), 1-7. https://doi.org/10.51317/eajk.v3i1.471

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 29.11.2023
Accepted: 31.01.2024
Published: 08.02.2024

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2024 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**
Makala hii iliazimia kuhakiki matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kukuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini* ya Clara Momanyi. Madhumuni ya karatasi hii ni kuchanganua namna mbinu ya umajazi wa kitashtiti umetumiwa kuwakuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umuundo. Wataalamu kama Scholes na Olsen wanashikilia mawazo kwamba ni muhimu kutumia Umuundo katika uhakiki wa maandishi ya fasihi kwa sababu lugha na fasihi zina uhusiano mkubwa sana. Matumizi ya Umuundo katika uhakiki wa fasihi hutuelekeza kuitazama fasihi kama mfumo ambao unajumlisha vipengele kama: Fani na maudhui ambavyo huchangia ukamilifu wake. Vipengele hivi huchangiana na kukamilishana katika kazi ya fasihi kama vile riwaya. Nadharia hii ya Umuundo ilitusaidia kuhakiki namna mbinu ya umajazi wa kitashtiti umetumiwa kusawiri wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Ukusanyaji wa data ulifanyika maktabani. Riwaya teule na makala zinazohusiana na mada zilisomwa. Data zilidondolewa, zilichujwa, zilichunguzwa na kisha zilichanganuliwa kwa kutumia majedwali na asilimia ya majina ya majazi ya kitashtiti. Data zilizokusanywa pia zilitumiwa kuhakiki matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika kuwakuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Pia, tuligundua kwamba mbinu ya matumizi ya umajazi wa kitashtiti yana mchango mkubwa kuwasawiri wahusika na kuyaendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Aidha, matokeo ya utafiti huu yatasaidia wahakiki, waandishi, walimu na wanafunzi wa shule za upili na hata vyuoni kuhakiki matumizi ya majina ya kimajazi katika kazi za fasihi andishi. Mbali na kazi hii kuwafaidi wahakiki, matokeo ya utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa katika kuwahamasisha waandishi chipukizi kutumia mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika harakati zao za utungaji riwaya.

**Maneno muhimu:** Maudhui, riwaya, tashtiti, umajazi, umuundo, wahusika.

**UTANGULIZI**

Riwaya ni mojawapo ya utanzu wa bunilizi. Huu ni utungo wa kinathari unaosimulia kisa kimoja au visa kadhaa, wenye upana wa kimawanda na kiwakati, uchangamano wa kimtindo na kidhamira na kina cha uhusika kinachohusisha undani wa kisaikolojia na ubainishaji wa misukumo ya kitendaji na wenye urefu wa kiasi fulani (Wamitila, 2008).

Wahusika katika kazi za fasihi wanaweza kusawiriwa kwa njia nyingi kutegemea msanii. Wamitila (2008) ameelezea mbinu kadhaa. Kwanza, anasema wahusika wanaweza kusawiriwa kwa mbinu ya kisimulizi ambapo mhusika anasawiriwa kwa usimulizi. Pili, ni mbinu ya kidrama, ambayo huwaonyesha wahusika wakitenda matendo na kuzungumza. Tatu, ni mbinu ya uzungumzi nafsia ambayo ni mtindo wa kuyawasilisha mawazo ya mhusika kwa mtindo au njia ya kujizungumzia. Nne, ni mbinu ya kisitiari ambayo ni ulinganishi wa moja kwa moja ambao hautambulishwi na matumizi ya maneno: kama, mfano wa, tamthili, mithili, ja n.k. Tano, ni mbinu ya kimajazi. Hii ni mbinu ya kutumia majina ambayo hufumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Hii ni mbinu ambayo inamrahisishia msomaji kazi ya kuwaelewa wahusika wanaopatikana katika kazi inayohusika (Wamitila, 2008). Majina haya ya kimajazi huwa mafumbo yanayoashiria maana, kwa mfano, Hasidi, Kazibure, Huzuni, Majivuno au Mashaka. Si kila mwandishi huyatumia majazi. Majazi ni mbinu ya kutumia majina ambayo hufumbata sifa za wahusika wanaopatikana katika kazi ya fasihi. Kwa upande mwingine umajazi wa kitashtiti ni mbinu ambayo mwandishi hujenga majina ya wahusika kwenye msingi wa kitashtiti. Mwandishi hutumia mbinu hii kufichua uovu au ujinga uliopo katika jamii (Wamitila, 2008).

Umajazi wa kitashtiti ni mbinu muhimu katika kazi za Kifasihi. Hulenga kufichua matendo mabaya katika jamii ya mtunzi. Mbinu ya umajazi wa kitashtiti hutumia mbinu ya kinaya, ucheshi au kejeli katika harakati za kufichua uozo katika jamii. Mbinu hii ya kitashtiti ilianza kutumiwa na wasanii wa Kigiriki. Watunzi walitumia mbinu hii kwa kiasi kikubwa. Waliotumia mbinu ya kitashtiti ni kina Aristophanes sawa na Mshairi Horace ambaye alitumia mbinu hiii sana katika ushairi wake (Senkoro, 1982). Mtunzi wa kazi za fasihi anaweza akatumia mbinu ya umajazi wa kitashtiti ama kwa majina ya wahusika au majina ya mandhari katika kazi ya fasihi. Kwa mujibu wa makali hii, umajazi wa kitashtiti ulitumiwa kwa maana ya majina ya wahusika yanayodhihirisha kinaya cha maana ya majina yao katika riwaya ya *Tumaini*.

Kwa hivyo, utafiti huu ulilenga kuhakiki matumizi ya umajazi wa kitashtiti katika kuwasawiri wahusika na kukuza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Utafiti huu unatoa muhtasari wa riwaya ya *Tumaini* na kisha unangazia wahusika watatu: Waridi, Almasi na Mwalimu Majaaliwa waliosawiriwa kwa kutumia umajazi wa kitashtiti na namna wanavyochangia kuendeleza maudhui kupitia mbinu hii ya kipekee.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

**Misingi ya Nadharia**

Nadharia ya Umuundo ilikuwa tokeo la upanuzi wa nadharia ya lugha ya Ferdinand de Saussure (1857-1913) kutoka kwa uchunguzi wa sentensi na kuitumia katika nyanja zingine kama Anthropolojia, utamaaduni pamoja na fasihi (Kaplan, 1986; Peck & Coyle, 1984). Umuundo una msingi wake katika Urasimu (Wamitila, 2002; New Encyclopaedia Britanica, 2003 na Scholes, 1974). Baadhi ya wataalamu waliohusika na Urasimu ni wale waliohusika na kuendeleza nadharia ya Umuundo, baadhi ya waatalamu hao ni kama vile: Roman Jakobson, Trubetzkoy, de Courtenay na Rene Wellek.

Uchunguzi zaidi wa Umuundo uliendelea katika miaka ya arobaini. Roman Jakobson alichangia katika kuasisiwa kwa kikundi cha isimu cha New York kilichowahusisha watu kama Claude Levi-Strauss; mwana-anthropolojia ambaye mawazo yake yamekuwa na athari kubwa katika nadharia ya Umuundo.

Scholes (1974) na Olsen (1973) wanashikilia mawazo kwamba ni muhimu kutumia Umuundo katika uhakiki wa fasihi kwa sababu lugha na fasihi zina uhusiano mkubwa sana kwani fasihi hutumia lugha kama nyenzo ya kuyapitishia maudhui ya wasanii. Mhakiki wa kimuundo anapaswa kutambua vipengele mbalimbali vinavyoujenga mfumo unaotawala matumizi ya

nadharia ya Umuundo na namna ya kuviunganisha (Jefferson & Robey 1986).

Nadharia ya Umuundo husisitiza vipengele vya kazi ya sanaa, jinsi vinavyohusiana hadi kuikamilisha kazi ya fasihi. Nadharia hii haiangalii kila kipengele peke yake lakini huangalia mahusiano yaliyoko baina ya vipengele vyote. Vipengele huhusiana kama viunganisho vya mkufu na huamua uhusiano wao (Scholes, 1974 & Wafula na Njogu (2007). Kutokana na maelezo haya, utafiti huu uliangalia fani ya lugha ya kimajazi ilivyochangia kufafanua wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*.

Msokile (1993) anasema kazi ya sanaa kwa mkabala huu huangaliwa kama kitu kisichohusiana na jambo jingine nje ya kazi yenyewe. Mhakiki huikabili kazi ya kifasihi kwa kuchunguza vipengele vya kazi hiyo na kuona jinsi vinavyohusiana.

Baada ya kuipitia mihimili ya nadharia ya Umuundo kwa mujibu wa utafiti huu ilidhihirika kwamba baadhi ya mihimili haiwezi kufaa katika uhakiki wa kazi za kifasihi zenye mwelekeo wa kimuktadha au unaozingatia nafasi ya msomaji na mtunzi wa kazi husika. Hata hivyo, baadhi ya mihimili ni muhimu na ndiyo maana utafiti huu uliteua nadharia hii kama nguzo ya kuchunguzia suala la utafiti kwa msingi huu wa kinadharia, utafiti huu ukazingatia baadhi ya mihimili ya Umuundo. Mihimili mikuu ya nadharia ya Umuundo katika makala hii ni kama ifuatayo:

i) Nadharia ya Umuundo huangalia kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza. Mhimili huu ulifaa kwa kuangalia namna kipengele cha wahusika kinavyosaidia kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*.

ii) Umuundo husisitiza fani ya kazi ya sanaa. Hii hujumuisha mbinu za masimulizi, muundo wa hadithi au ushairi, lugha ilivyotumika mfano msamiati na uteuzi wake, majazi, takiriri, tashibiha, istiari n.k.

iii) Kama ambavyo muundo wa lugha ni mfumo, muundo wa fasihi una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine. Hakuna kipengele cha fasihi kati ya hivyo kitakachoelezwa vizuri katika upekee wake. Kwa hivyo katika makala hii, tutaangazia mahusiano hayo baina ya matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kukuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*.

iv) Sanaa inajisimamia yenyewe na ni chombo kinachojitosheleza, kisichobadilika na kuwa inaendelea. Kwa hivyo hamna haja kutumia mambo ya nje kuhakiki kazi ya fasihi. Katika utafiti huu data za kimsingi zitatokana na uchanganuzi wa matini za riwaya ya *Tumaini*.

Kwa kuegemea mihimili hiyo mahususi, makala hii ilihakiki matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kukuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Riwaya ya *Tumaini*

Masimulizi ya riwaya hii ya *Tumaini* yanamnzunguka mhusika mkuu anayeitwa Tumaini. Anwani ya riwaya imetokana naye. Tumaini alizaliwa katika jamii inayozingatia utamaaduni na kaida za kale. Ni jamii iliyojaa taasubi za kiume. Jamii ambayo mwanamume ndiye anayetoa maamuzi yote yanayoathiri jamii. Mwanamume ndiye mwenye sauti na mwanamke ndiye kusikia sauti za mwanamume na kufuata maamuzi ya mwanamume. Mwanamke alihitajika kuonekana tu hawakutarajiwa kuongea wala kudhihirisha mahitaji na matamanio yao. Tumaini alilelewa katika mazingira hayo ya kunyanyaswa kwa wasichana na wanawake.

Tumaini alikuwa msichana mchanga ambaye alikuwa bado anasoma katika shule ya msingi. Babake alikuwa Mzee Masumbuko ambaye mtunzi amemsawiri kama mtu mwenye hamaki na sura ya kutisha (uk 2). Mamake alikuwa anaitwa Amina na Tumaini alikuwa na dada zake wawili, Rehema na Mashaka pia na kaka mmoja aliyeitwa Idi. Tumaini alikuwa na ujasiri wa kipekee na alijitokeza kama kijana wa kike aliyekuwa na mazoea ya kudadisi utamaduni wa jamii yake, hasa imani na mila ya wasichana kukeketwa na kuozwa mapema.

Mwanzoni mwa riwaya, mtunzi anatuonyesha Tumaini akiwa katika harakati zake za kutoroka nyumbani

kisirisiri. Katika sura ya kwanza, mwandishi anamsawiri Tumaini akitoka nyumbani kwao na kushika safari yake hadi kwa Shabani na Halima. Tumaini anapofika mle anajaribu kujieleza kuhusu kutoroka kwake nyumbani kwao. Mtunzi anatumia kisengere nyuma kutufahamisha kuhusu maisha ya awali ya shuleni na matarajio ya Tumaini. Baadaye Idi alifika kumtafuta na kumweleza kwamba babake alikuwa amekasirishwa na kupotea kwake. Kupotea kwa Tumaini kulimsumbua sana Mama yake Bi. Amina.

Hata hivyo, baada ya mabishano na mashauri, Tumaini anaanza maisha mapya kwa Bwana Shabani, anapata nafasi ya kuendelea na masomo yake, licha ya vijana kuendelea kumletea pesa mzee Masumbuko. Mpango wa Mzee Masumbuko wa kupanga kumwoza Tumaini kisirisiri unatibuka. Mzee Masumbuko alijikaza kwa juhudi sana na mtunzi anasema alikuwa amefika kiwango cha kumhonga chifu Andrea. Chifu Andrea alikosa kuwajibika kama mtumishi wa serikali na kukubali kushinikizwa na mzee Masumbuko. Mienendo ya chifu Andrea inaenda kinyume na sheria za nchi.

Licha ya shida anazozipitia Tumaini, aliendelea kujikakamua katika masomo yake kwa bidii na matumaini mengi. Anapokamilisha masomo yake ya shule ya msingi na kufanya mtihani, matokeo ya mtihani yanapotolewa, Tumaini anaibuka kufanya vyema na kujiunga na shule ya upili. Alipambana hadi akapata ufadhili na akaendelea hadi akakamilisha masomo ya shule ya upili baada ya miaka minne. Rehema, dada yake Tumaini, hana bahati nzuri kwani anaozwa mapema kwa fundi wa baskeli. Rehema alipoingia maisha ya ndoa alipata shida chungu nzima, jambo ambalo lilimsumbua Tumaini. Aidha, mtunzi anagusia maisha ya Majuto na tabia zake mbaya kama vile wizi. Tabia yake ya wizi ilimpelekea kupigwa risasi na kuwekwa gerezani miaka minne.

Kwa ujumla, riwaya hii ya *Tumaini* kwa ubunifu na kwa undani inashughulikia suala zima la malezi linajumuisha ulezi wa baba mwenye kuongozwa na mawazo wa taasubi za kiume na mtazamo hasi kuhusu maisha ya wasichana. Mtazamo ambao ulipitwa na wakati na hauna nafasi katika ulimwengu wa kisasa. Mtazamo huo unapigwa vita na Tumaini na wahusika wengine kama bwana Yusufu, bwana. Shabani, Amina na Halima, D.O na wengine. Tumaini anaibuka mshindi na kufanikiwa kufuata ndoto yake ya masomo. Tumaini aliamua kufanya masomo ya sayansi katika chuo kikuu kinyume na matarajio ya wanaume wenye kasumba ya taasubi ya kiume kama mwalimu mkuu Bw. Majaaliwa. Riwaya hii ya *Tumaini* inawapa shime na kuwamotisha wasichana wengi wanaopititia changamoto za mila na desturi za kijadi kujikwamua ili waweze kufuata ndoto zao na kufikia malengo yao ya maisha. Utafiti huu una uhusiano na ule wa Ndung'u (1996), ambaye alishughulikia uhakiki wa fani katika riwaya zifuatazo za Katama Mkangi: *Ukiwa, Mafuta* na *Walenisi.* Alichanganua jinsi baadhi ya wahusika wameumbwa na majukumu yao katika riwaya hizo. Vilevile aligusia mbinu zilizotumika kuwaumba wahusika katika riwaya teule za Katama Mkangi kama vile mbinu za kidrama, majazi na nyinginezo. Hata hivyo, Ndung'u kinyume na utafiti wetu, aliangazia tu namna wahusika walivyosawiriwa na mtunzi na majukumu yao bila kuhusisha na maudhui katika kazi riwaya zake.

## Majina ya Umajazi wa Kitashtiti katika Riwaya *Tumaini*

Makala hii iliazimia kuhakiki matumizi ya mbinu ya umajazi wa kitashtiti katika kukuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini* ya Clara Momanyi. Madhumuni ya karatasi hii ni kuchanganua namna mbinu ya umajazi wa kitashtiti umetumiwa kuwakuza wahusika na kuendeleza maudhui katika riwaya ya *Tumaini*. Karatasi hii inaangazia wahusika watatu: Waridi, Almasi na Mwalimu Majaaliwa waliosawiriwa kwa kutumia umajazi wa kitashtiti na namna wanavyochangia kuendeleza maudhui kupitia mbinu hii ya kipekee

### 1. Waridi

Waridi ni ua mojawapo linalonukia na huwa ya rangi mbalimbali: Ua la waridi, Waridi huvutia watu wengi kwa sababu ya kupendeza macho na harufu yake nzuri *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (2014). Kwa hivyo, wasomaji na wahakiki wa riwaya ni lazima kuyachunguza majina ya kimajazi na kuyahusisha na maudhui na ujumbe wa riwaya husika (Wamitila, 2010). Mbinu ya majazi, humwezesha mwandishi kufumbata sifa kuu za mhusika na huyafanya maudhui yawe wazi mbali na kuuonyesha msimamo wa mwandishi. Katika riwaya ya *Tumaini* mtunzi anatueleza kuwa Waridi alikuwa akisoma katika darasa moja na Tumaini katika shule ya kivulini. Waridi kinyume na Tumaini hakuwa akitilia maanani masomo yake. Kwa mfano, Waridi hakuwa akipenda somo la hisibati hata kidogo (uk 73). Shule kwake ilikuwa kama jela na mateso. Mtunzi anasema kwamba Waridi alikuwa akichukia shule kwa

sababu ilimfungia mambo mengi ya kupendeza zaidi huko nje. Alienda shule kwa sababu ya kulazimishwa na wazazi wake. Waridi alikosa motisha ya ndani kuhusu masomo yake, kwa hivyo kuhudhuria masomo kulikuwa na lengo la kutimiza tu matarajio ya jamii yake. Waridi hakuwa na malengo mahsusi katika masomo yake, aliendelea kuupitisha tu wakati shuleni huku akiwatania wanafunzi waliokuwa na shabaha shuleni kama Tumaini. Waridi kama mwenzake Almasi hakuwa na nia ya kufaulu shuleni. Madhumuni yake yalikuwa kuolewa na kuonja uhondo wa maisha nje ya shule. Daima alikuwa akiwatania kina Tumani na Vumilia kwa bidii ya masomoni (uk. 74). Waridi alilenga kuwavutia vijana wa kiume, haya yalidhihirika pale alipopigania kijana aliyeitwa Paulo na msichana mwingine aliyeitwa Masika (uk 111). Kile alichokijua yeye vizuri ni kujipodoa na kujiweka manukato ya kunukia kila wakati ili aweze kuwapendeza wenzake na hasa wavulana. Pia, Waridi alikuwa akiwasumbua wenzake darasani kwa mzaha na masimango. Huku akianguka mtihani na kupata sufuri ambazo aliziita mayai yake (uk 20). Majina ya majazi yanaishia kuwa kama ishara: yanatuelekeza kwenye tabia na wasifu wa wahusika wenyewe (Wamitila, 2010). Mwandishi anao uhuru wa kufanya uteuzi wa majina ya wahusika wake kutegemea maudhui yake, kwani maudhui huongoza fani (Mohamed, 1995). Katika hali hii, mwandishi huwasawiri wahusika wake wa kimajazi kwa kuongozwa na matakwa ya maudhui yake anayotaka kuyapitisha kwa wasomaji wake. Kwa mfano, ikiwa mwandishi analenga kuangazia maudhui ya imani, basi atateua na kumtumia mhusika Imani. Mtunzi atampa Imani tabia, mienendo na sifa zake zote zitachangia maudhui ya imani.

### 2. Almasi

Almasi ni madini ngumu ya thamani sana aghalabu huitumika kukatia kioo, mojawapo ya vito vya thamani (K*amusi ya Kiswahili sanifu*, 2014). Maisha ya Almasi yalikosa thamani shuleni na kukosa kung'aa kimasomo. Almasi alipenda sana kujikwatua na kujirembesha sana (uk 19) hakuyapenda masomo kama alivyopenda mapambo na unadhifu wa mwili. Mwalimu wake alimpa jina la Chaurembo. Ayodi (2011), aliangazia matumizi ya tashtiti katika tamthilia zifuatazo: *Amezidi, Mashetani, Usaliti Mjini na Mkaguzi Mkuu Serikalini.* Matokeo ya utafiti wake yalionyesha umuhimu wa mbinu ya kitashtiti katika kuwasilisha maudhui nyeti. Utafiti wake ulidhihirisha kwamba tashtiti ni mbinu mwafaka ya kuweka wazi na kurekebisha uovu na ujinga katika jamii kwa njia ya ucheshi. Almasi hakuwa na thamani yoyote katika nyanja za masomo na hakujua kwamba bila masomo maisha yake yangekosa thamani siku za usoni.

Kama Waridi alimchukia pia mwalimu wa hisibati. Alikuwa amekufa moyo na hakuwa na matumaini ya kufanya vyema katika masomo yake. Alikuwa akipitisha siku tu shule na shughuli zake za kisomo zilikuwa za kutimiza tu (uk 74). Alikuwa amechoka kweli na masomo yake. Mtunzi anadhihirisha kwamba matumaini ya kufanikiwa katika maisha hayapatikani kutokana na urembo wala sura ya mwili. Lakini maisha mazuri kwa wasichana hutokana na juhudi na bidii zao shuleni. Almasi alipotoshwa na uhondo wa maisha nje ya shule. Kwake yeye, maisha yalipata thamani na maana yake kutokana na urembo na kujikwatua kila mara, yeye alipuuza mambo muhimu katika maisha yake. Alisahau kwamba masomo na elimu bora ndiyo msingi dhabiti ya katika maisha ya binadamu. Alikosa mwelekeo mzuri.

Kawika (2011), amefanya utafiti kuhusu wahusika katika fasihi simulizi za kisasa. Alishughulikia baadhi ya hadithi kutoka kazi zifuatazo: *Kicheko Cha Ushindi* (1978), *Pendo la Heba na Hadithi Nyingine* (1996) na *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004). Utafiti wake ulidhihirisha kuwa wahusika katika hadithi fupi za Kiswahili huwa wakamilifu na watoshelevu, yaani wahusika wanatosheleza katika kutumiwa kama nyenzo za kuyapitisha dhamira na maudhui ya waandishi. Mtunzi amemtumia Almasi kuthibitisha kwamba King'aacho si dhahabu kila wakati. Sifa za Almasi zilikuwa za nje tu lakini ndani yake ni ombwe tupu, alikuwa mjinga na mwenye kupuuza mambo muhimu shuleni kama masomo yake na kumakinika vilivyo. Nadhari yake masomoni ilipotoshwa na marafiki, raha na mzaha wa ujana wake.

### 3. Mwalimu Maajaliwa

Maajaliwa ni mambo yatokanayo na rehema za mwenyezi Mungu. Mapenzi ya mwenyezi Mungu; jacha, kadari, kiduru, takdiri (*Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, 2014) kitaaluma mwalimu maajaliwa alikuwa mwalimu mkuu wa Milimani Mission School, kazi na cheo ambacho alitarajiwa kukitumia vizuri kuwashauri, kuwaelekeza na kuwamotisha wanafunzi kuyafikia malengo yao mahsusi katika maisha yao. Bwana Maajaliwa amesawiriwa na mtunzi kama mwalimu mkuu asiye na busara na mwenye mwelekeo hasi kuhusu uwezo wa wanafunzi wake hasa wasichana (uk 115). Jina lake ni maajaliwa lakini hakujaliwa hekima katika maisha yake hakutunukiwa uwezo wa kuyagusa maisha ya watu wengine kwa njia ya matumaini. Uchunguzi wa

majina ya wahusika lazima uhusishwe na dhamira na maudhui katika kazi inayohusika (Wamitila, 2002). Katika muktadha wa utafiti huu, kipengele kimoja cha fani katika riwaya ndicho kiliangaziwa: wahusika. Wahusika wenye majina ya kimajazi walishughulikiwa na namna wasanii wanavyowatumia kuendeleza maudhui yao katika riwaya ya *Tumaini*.

Mwalimu Maajaliwa aliwakataza wanafunzi kujaza masomo ya sayansi kwenye fomu za vyuo vikuu. Mtunzi amemtumia Maajaliwa kuonyesha kuwa katika maisha vikwazo na vizingiti vinaweza kutokea lakini havitazuia juhudi zetu za kufikia malengo yetu ya maisha. Bwana Maajaliwa, anayaendeleza matokeo ya sifa za jina lake la kimajazi. Fani na maudhui ni vipengele ambavyo huenda pamoja, kimoja kikisaidia kingine. Kwa maneno mengine fani na maudhui huchangiana na huingiliana (Mohamed, 1995). Maoni haya yanaonekana kwenda sambamba na yale ya Reeves (1956) ambaye alisema kuwa katika kazi yoyote ya sanaa, fani na maudhui haviwezi kutenganisha. Mungu hawezi akajalia mja sifa ya roho ya kukosa matumaini na kukosa imani ya watu wengine ambao pia ni waja wa Mungu.

**Jedwali 1: Mandhari na Wahusika wenye Majina ya Umajazi wa Kitashtiti na Maudhui Wanaoyaendeleza Riwaya ya *Tumaini;***

| **Riwaya** | **Maudhui** | **Wahusika Wanaoyaendeleza** |
|---|---|---|
| *Tumaini* | Malezi<br>Elimu | Almasi Na Waridi.<br>Mwalimu Maajaliwa, Almasi, Waridi. |

Kwa mujibu wa jedwali hapo juu, inadhihirika kuwa mtunzi wa riwaya ya *Tumaini* amewatumia wahusika wawili tu wenye majina ya umajazi wa kitashtiti kuyaendeleza maudhui yake. Haya yanathibitisha yanayosemwa na Chimerah na Njogu (1999) kuwa wahusika hujadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na maudhui na hili hujitokeza kutokana na maneno au matendo yao. Katika kazi ya fasihi hulka ya wahusika hujitokeza kupitia kwa maelezo ya msanii au kwa kutazama kwa undani maneno au matendo yao katika kazi ya sanaa. Aidha, mtunzi amewatumia wahusika watatu, yaani, Almasi, Waridi na Mwalimu Maajaliwa kuyaendelezea maudhui yake. Waridi na Almasi wametumiwa kuyaendeleza maudhui ya malezi na elimu, huku mwalimu Maajaliwa ametumiwa kuyaendeleza maudhui ya elimu. Wamitila (2008) anasema kuwa whusika ni muhimu katika kazi ya kifasihi kwa kuwa huwa watendaji wakuu wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira na maudhui ya kazi yenyewe. Kwa hivyo, inadhihirika kwamba ijapokuwa mtunzi amewatumia wahusika watatu kuyaendelezea maudhui yake, kunao uhusiano mkubwa kati ya maudhui na wahusika katika riwaya ya *Tumaini*. Wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti wametumiwa na mtunzi kuyaendeleza maudhui yake.

## HITIMISHO

Kwa kuhitimisha, katika sehemu hii tumeweza kuonyesha namna wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti wametumiwa na mtunzi wa riwaya ya *Tumaini* kuyaendeleza maudhui yake. Mtunzi amewasawiri wahusika wenye majina ya umajazi wa kitashtiti kuyaendeleza maudhui ya elimu na malezi. Aidha, ilibainika kwamba mtunzi wa riwaya ya Tumaini hakuyatumia majina ya mandhari ya umajazi wa kitashtiti kuyaendelezea maudhui yake.

## MAREJELEO


Ayodi, N. (2011). *Matumizi ya Tashtiti katika Tamthilia Teule za Kiswahili*. Tasnifu ya PhD Chuo kikuu cha Egerton (Haijachapishwa).

Chimera, R., & Njogu, K. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*, Jomo Kenyatta Foundation.

Hawkes, T. (1977). Structuring and Semiotics, Methuen.

Jefferson, A., & Robey, D. (1986). *Modern Literary Theory*. Batsford Ltd.

Kamusi Sanifu ya Kiswahili (2014). *TUKI*.

Kaplan, C. (1986). *Criticism: The major Statements*. St. Martins Press.

Kawika, M. (2012). *Wahusika katika Hadithi Fupi za Kisasa za Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili Chuo kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa.).

Mohamed, S. (1995). *Kunga za Nathari ya Kiswahili.* East Africa Educational Publishers.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Vide-Muwa Publishers Ltd.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. University Press.

Ndungu, N. (1996). *Uhakiki wa Fani katika Riwaya za Katama Mkangi.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Peck, J., & Coyle, M. (1984). *Literary Terms and Criticism*: Macmillan Educational Books.

Reeves, J. (1956). *The Critical Sense, Practical Criticism of Prose and Poetry*. Heinemann.

Scholes, R. (1974). *Structuralism: An Introduction*. Yale University Press New Haven.

Senkoro, F. (1982). *Fasihi Dar es Salaam*: Press and Publicity Centre.

Wafula, R. na Njogu, K (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Nairobi JKF.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake.* Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*: Focus books Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Kazi ya Fasihi 1 Misingi ya Uchaganuzi wa Fasihi Nairobi*: Vide- Muwa Publishers.